

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA KUMI NA NANE**

**30 APRILI, 2019**



## **ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

### **MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA KUMI NA NANE – TAREHE 30 APRILI, 2019**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA MAJI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.



**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**146. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itakarabati Shule ya Sekondari ya Mpanda *Girls*.

## **WIZARA YA NISHATI:**

### **147. MHESHIMIWA RASHID AJALI AKBAR (NEWALA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-  
Takwimu zilizopo zinaonesha kuwa gesi kutoka Mtwara na Songosongo inatumika kwa asilimia sita tu:-

- (a) Je, kwa nini Kiwanda cha Saruji cha Dangote na Mtwara *Cement* Mkoani Mtwara havijapatiwa umeme wa gesi asilia hadi leo;
- (b) Je, kwa nini Wananchi wa Mtwara wasiunganishiwe gesi asilia kwenye nyumba zao.

## **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

### **148. MHESHIMIWA ALEX RAPHAEL GASHAZA (NGARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Zamani kulikuwa na maeneo

yaliyokuwa yametengwa kwa ajili ya Mifugo na Kilimo katika kutekeleza Sera ya matumizi bora ya ardhi, lakini kadri idadi ya watu inavyoongezeka maeneo hayo yanavamiwa na kusababisha migogoro:-

Je, Serikali ina mpango gani juu ya kuanzisha Skimu ya ufugaji wa kisasa utakaozingatia Kanuni za ufugaji bora na kilimo cha kisasa ili kuepukana na migogoro ya Wakulima na Wafugaji.

**WIZARA YA KILIMO:**

**149. MHESHIMIWA RICHARD PHILIP MBOGO (NSIMBO):**

● Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

(a) Je, ni lini Serikali italeti mbegu bora ya Tumbaku kama inayolimwa katika nchi nyingine Kusini mwa Jangwa la Sahara;

(b) “*Produce cess*” ilishushwa toka 5% mpaka 3% ili Mkulima afaidike kwenye bei ya kuuza lakini hakuna utekelezaji kwa Makampuni ya kununua Tumbaku na kwenye Halmashauri mapato yameshuka; Je, Serikali inaweza kupitia upya Sheria hiyo na kurudisha kama awali;

(c) Je, ni lini Serikali itakaribisha Kampuni nyingine za kununua Tumbaku ili kuongeza ushindani na kuondoa hofu kwa Wakulima.

## **WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

### **150. MHESHIMIWA JANET ZEBEDAYO MBENE (ILEJE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Serikali ilinunua mashine ya kujengea kutoka Marekani kwa fedha nyingi sana kwa lengo la kuitumia kujenga nyumba nyingi za Watumishi, Ofisi na Taasisi n.k. kwa haraka zaidi, mashine hiyo kwa muundo wake ina uwezo wa kujenga nyumba kwa bei nafuu zaidi na hivi sasa kuna upungufu mkubwa wa nyumba za Walimu, Madarasa, Maabara, Mabweni, Nyumba za Wauguzi, Madaktari na

- Vituo vya Afya:-
  - (a) Je, ni nyumba ngapi na kwa gharama gani zilizojengwa na Jeshi la Ulinzi na Kujenga Taifa kwa kutumia mashine hiyo na kama zingejengwa kwa ujenzi wa kawaida zingetumia kiasi gani;
  - (b) Je, ni kwa nini mashine hiyo haitumiki kujenga nyumba zinazohitajika wakati kuna upungufu mkubwa sana wa nyumba za Serikali;
  - (c) Je, Serikali iko tayari kufanya tathmini na kutuletea Bungeni mpango mzima wa kuanza kutumia mashine hiyo kujenga nyumba zinazohitajika.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **151. MHESHIMIWA BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA (CHWAKA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Mara nyingi wakati wa chaguzi mbalimbali Zanzibar kunajitokeza hali ya fujo na ukosefu wa amani na kusababisha Wananchi kukosa amani na wakati mwingine kutoshiriki katika chaguzi husika:-

Je, Serikali inawaambia nini Wananchi wa Zanzibar juu ya suala hilo.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **152. MHESHIMIWA MWANNE ISMAIL MCHEMBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Tabora Manispaa kuna Zuu ya Wanyama wapole ambayo ilitengwa muda mrefu na mpaka sasa wanapungua na kuifanya Zuu hiyo kukosa maana:-

Je, Serikali iko tayari kupeleka Wanyama hao katika Zuu hiyo.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**153. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo watoto wengi njiti huzaliwa; na akina mama wanaojifungua watoto hao njiti wengi wao ni waajiriwa ambao hupata changamoto ya likizo ya uzazi inayotosha kwa malezi ya awali ya watoto hao njiti:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha akina mama hao wanaongezewa likizo ya uzazi;
- (b) Akina mama hao wanapojifungua pia hupata changamoto ya vifaa kama vile vifaa vya kukamulia maziwa, dawa na gharama za matibabu; Je, Serikali imejipangaje kuwasaidia gharama za vifaa hivyo;
- (c) Je, Serikali ina mpango gani wa kudumu wa kutokomeza suala la akina mama kuzaa watoto njiti.



#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
30 APRILI, 2019**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**

